

Nakuandikia kukukaribisha kushiriki mukutano wa jiji utakaofanyika kwa mawasiliano ya hewani kuhusu upingaji wa ukandamizi dhidi ya watu weusi Vancouver, mchanganuo wake huu ufuatao:

Tarehe: 12-2 jioni siku ya Alhamisi, Septemba 24

Wapi: [Mukutano kwa mfumo wa video](#) kama utataka kushiriki

Tazama: Mukutano wa jiji utapeperushwa kuititia [YouTube](#) kama utapendelea kutazama tukio badala ya kushiriki kikamilifu

Mukutano wa jiji umeandaliwa na jiji la Vancouver na kuratibiwa na mwanaharakati wa jamii Vanessa Richards. Tunakukaribisha kuungana nasi katika tukio hili katika jitihada za ushirikiano kusaidia kutengeneza jiji ambamo kila mmoja atastawi.

Wakati wa mukutano, Meneja wa jiji, Sadhu Johnston na mimi tutazungumzia kwa kina mapendekezo na mchanganuo wa mambo tuliyo shirikishwa na watu weusi na waAfrika wanaoishi ughaubuni. Tunatambua kuwa katika kazi hii tunajifunza na siyo viongozi.

Lengo letu ni kukupatia nafasi ya kuchangia mawazo, vipaumbele, wasiwasi, na matarajio yako wakati tukiainisha hatua zifuatazo tunazohitaji kukamilisha kukidhi haja hizi.

Tunakukaribisha na kutilia mkazo muelekeo wetu katika mukutano huu wa jiji kwa watu weusi na waAfrika waishio ughaubuni ili kuweka katikati sauti na mitazamo yao kuititia tukio hili na ninatumaini utashiriki. Tukio hili ni hatua muhimu katika kufanyakazi pamoja kuunda shirika ambalo linashirikisha jamii kutengeneza haki, usawa, utofauti, ujumuishaji na uwajibikaji.

Tunakuhimiza kushiriki maswali na maoni yako mapema. Hii itahakikisha kuwa sauti nydingi iwezekanavyo zinasikika: Maswali yanaweza kuwasilishwa kwa:

- Barua pepe equity@vancouver.ca
- [Tembelea tovuti ya jiji](#) ambayo pia ina maelezo kamili ya tukio hili.

Jiji limeazimia kujibu maswali yote tunayopokea, na yale ambayo hayajibiwi wakati mukutano wa jiji yatajibiwa kuititia barua pepe baada ya tukio.

Ningependa vilevile kuchukua fursa hii kuwashukuru nyote kwa mapendekezo ya kina na maombi yote ambayo tayari mmeshatufikishia. Mapendekezo haya tayari yanatumika katika mfumo wetu wa utoaji maumuzi na katika kazi ya kukabiliano dhidi ya ubaguzi wa rangi. Muhtasari wa mapendekezo haya pamoja na kazi yetu kufikia sasa imeambatanishwa na barua pepe hii, pia unaweza kusoma zaidi kuhusu kazi ya jiji dhidi ya ubaguzi wa rangi kwa ujumla [hapa](#).

Naangalia mbele fursa ya mabadiliko na ushirikiano umbayo itatuvusha pamoja.

Naogopa hatukuweza kutoa tafsiri hapo kwa hapo wakati wa tukio kwa sasa lakini tunapenda kuhimiza familia zenye watu wanaozungumza lugha zaidi ya moja kusaidia kutafsri kingereza.

Tafadhali wasiliana name kama unalo swali lolote au jambo lolote kuhusu hili.

Ahsante,

Sandra Singh